

MATUMAINI PROG NO:2527

TITLE: AM I MY BROTHER'S KEEPER ?

SUMMARY: KIZUNGUMZIA KUHUSIANA NA MATOKEA YA KUACHANA NA MUNGU.

TEXT: MWANZO 4:1-16

MADA: MIMI NI MLINZI WA NDUGU YANGU?

.....

Hebu kwanza kabisa tukapate kuomba kabla ya kuendelea na somo hili la leo.
Natuombe;

OMBI....Mwenye Utukufu na mamlaka yote Mfalme wa Wafalme,,tunasema ni asante kwa sababu ya ulinzi na zaidi mno uwepo wako. Tunapolianza somo hili la leo ,,tunakuomba ukatuongoze ili tukapate kulielewa vyema. Ni kwa Yesu tumeomba, Amina.

Msikilizaji wangu,,Mungu wetu ametujalia tena kwa nafasi hii ambayo ni ya kujifunza kutoka kwenye neno lake ambalo ni Bibilia. Ni tumaini langu kwamba unaendelea vyema kabisa. Karibu tena kwenye somo letu la leo lenye Kichwa,, *,,,mimi ni mlinzi wa ndugu yangu?*

Kipindi hiki ni cha Matumaini kutoka TWR Kenya.
Somo ni kutoka kwenye Mwanzo 4:1-16 .

Kwa kulimalizia fundisho hili la leo,, nitakuwa na kupatia anwani yangu ya mawasiliano.

Kwanza kabisa uhapa wimbo,,Kaini na Abeli.....

WIMBO:

Asanteni sana wana-Khwisero SDA church kwa ujumbe huo kupitia kwa uimbaji.....
Mimi naitwa, Vincent Amara.

Msikilizaji wangu,,tunapofikiria juu ya nguvu kuu ya Mungu wetu, tunaweza kudhani kuwa angeweza kuumba taifa zima kwa mara moja, akiliamuru liwepo kama alivyofanya kwa wanyama katika Mwanzo 1.

Lakini kwa Mungu kuchagua kumuumba mwanamume mmoja na pia mwanamke mmoja Adamu na Hawa na kuwaambia hivi, "*Zaeni, mkaongezeke, mkaijaze nchi.*" Bila shaka Alitaka wawe familia na zaidi sana jumuiya.

Rafiki yangu,, neno linatuambia ya kwamba,,, baada ya muda,,, wawili hao walipata mtoto wa kiume, mzaliwa wa kwanza wa ulimwengu wa wanadamu, ambaye Hawa alimwita Kaini akisema, "*Nimepata mtu kwa Bwana.*"

Hakika wawili hawa,,, walitarajia mambo makubwa kutoka kwake. Kisha wakapata mtoto wa pili, Habili. Hivyo kukawa na ndugu wawili, Kaini na Habili.

Sasa, katika kitabu cha Mwanzo 4:1-16,,, tunakipata kisa hiki kizito ambacho kinatupelekea kwenye swali kuu ambalo ni ,,Je, mimi ni mlinzi wa ndugu yangu?

Tukiyarejelea maandiko kwenye Biblia katika kitabu cha Mwanzo 4:1-16 ambapo nitazisoma aya za kimsingi tu,,, yaani aya ya 8-10,,,

Neno linasema hivi;

8.Kaini akasema na Habili nduguye; ikawa walipokuwapo kondeni, Kaini akamwinukia Habili nduguye, akamwua.

9.Bwana akamwambia Kaini, "Yuko wapi Habili nduguyo?" Akasema, "Sijui; mimi ni mlinzi wa ndugu yangu?"

10.Akasema, "Umefanya nini? Sauti ya damu ya nduguyo inanililia kutoka katika ardhi."

Ndugu pamoja na dadangu,,, kupitia maisha ya Kaini, tunapata kuona pande tatu kuu ambazo tunapaswa kuzitumia,, kujiangalia na kuyapima maisha yetu wenyewe leo, bila kutumia vichwa vya habari vya hapa na pale.

Upande wa kwanza tunaojionea ni,,, *Kaini Katika Kazi Yake.*

Kabla ya dhambi kuingia, Mungu alikuwa na urafiki sana na mwanadamu kule bustanini. Lakini baada ya uasi, ardhi ililaaniwa ikazaa miiba na mwanadamu akalazimika kula kwa jasho na machozi.

Neno linatuambia Kaini alikuwa mkulima,,, na bila shaka,,, mkulima stadi kwenye udongo uliokuwa na rotuba tele. Ndugu yangu,, kazi ya Kulima ni ya kuheshimiwa

tangu mwanzo. Kaini alifanya kazi kwa bidii na mazao yake yakasitawi, huku nduguye Habili akiwa mchungaji wa kondoo.

Kama *mwanatheolojia Matthew Henry* alivyowahi kusema,,, kazi au hali ya maisha iliyo bora zaidi kwetu, ni ile iliyo bora kwa nafsi zetu; ile inayotuepusha na dhambi na kutupa nafasi kubwa ya kumtumikia na kumfurahia Mungu. Swali kuu kwetu hapa ni kwamba,,Je, kazi unayoifanya inampendeza Mungu wetu? Na Je, umechagua kazi inayomheshimu Muumba wako?

Kipengele cha pili ndugu yangu,,, tunamwona,,, Kaini Katika Ibada Yake. Baada ya mavuno, kulikuwa na msukumo ndani yao wa kumtolea Mungu dhabihu ya kushukuru. Walikuwa wanaishi nje ya bustani ya Edeni, lakini bado walikuwa na ufahamu kamili wa uwepo wa Mungu kutokana na mafundisho ya wazazi wao.

Kaini alileta mazao ya ardhi kuwa sadaka, na Habili akaleta wazao wa kwanza wa kondoo wake na mafuta yake. Lakini Biblia inasema Bwana akamtakabali Habili na sadaka yake, bali Kaini na sadaka yake hakumtakabali.

Dadangu,,wasomi wa mambo ya kitheolojia wanaonyesha kuwa Habili alitoa sehemu zilizo bora zaidi za wanyama wake,,, jambo lililoonyesha utii na kujitolea kwa moyo wake wote kwenda kwa Mungu. Kaini, kwa upande mwingine, alitoa tu sadaka ya mazao kama mazoea, bila unyenyekevu wa kweli moyoni na tena sadaka isiyo na damu,,, jambo lililomfanya mwishowe aangukie kwenye dhambi.

Mpendwa,,, hebu tupime ibada zetu leo. Je, ibada yetu inampendeza Mungu? Je, tunaleta sadaka na mioyo ambayo Mungu anaweza kuziheshimu, au tunafanya ibada za mazoea tu?

Kipengele cha tatu na cha mwisho kwa leo kutokana na fungu hili,,, tunamwona,,, Kaini Katika Ulimwengu Wake.

Huu ulikuwa ulimwengu mdogo wa watu wachache sana,, yaani wazazi wao na ndugu zake wawili yaani Habili na Sethi.

Walipokuwa mashambani peke yao, chuki ya Kaini ililipuka,,, akamwinukia Habili nduguye na kumwua kinyama ili tu amwondoe mtu ambaye matendo yake ya haki yalikuwa yanamuhukumu.

Hapo ndipo tunapoona jinsi asili ya mwanadamu ilivyoharibika baada ya kutengana na Mungu. Ardhi ikanywa damu ya mtu wa haki iliyomwagika kwa

hasira. Katika Waraka wa 1 Yohana 3:12,,, neno linalotumika hapo linaashiria kuchinja kinyama kabisa. Kaini alikuwa mkatili na mnyang'anyi.

Mungu alipomuuliza, "Yuko wapi Habili nduguyo?" ili kumpa nafasi ya kutubu, Kaini alidanganya na kujibu kwa dharau: Alijibu hivi "*Sijui*; mimi ni mlinzi wa ndugu yangu?" Haba tunaweza kusema ya kwamba,,, alijaribu kukwepa wajibu wake. Alimlaumu Mungu kwa kutenda isivyo haki akisema, "Adhabu yangu ni kubwa isiyochukulika."

Lakini mstari wa mwisho unabeba neno la kutisha sana rafiki yangu,,mstari huo unasema kwamba "Kaini akatoka mbele za uso wa Bwana." Fikiria jambo hili; mzaliwa wa kwanza wa wanadamu anakuwa muuaji na anaondoka kwenda ulimwenguni pasipo Mungu! Maisha yake yakawa: Kazi ya kuheshimiwa, ibada isiyokubalika, na ulimwengu usio na Mungu!

Rafiki yangu , hebu tafakari kuhusu ulimwengu wako leo. Je, kazi zako ni za heshima? Je, ibada yako inakubalika? Na Je, Mungu anaheshimiwa na kuongoza maisha yako?

Na zaidi ya yote,,Mruhusu Bwana anene na moyo wako kuhusu lile swali la Kaini ya kwamba; Je!, mimi ni mlinzi wa ndugu yangu"?"

Halafu je!,,wewe unawajibika kwa ajili ya ndugu zako!

Ningependa kukuacha na neno hili la Kutia Moyo kutoka 1 Petro 2:9 linalosema,,, "Bali ninyi ni mzao mteule, ukuhani wa kifalme, taifa takatifu, watu wa milki ya Mungu, mpate kuzitangaza fadhili zake yeye aliyewaita mtoke gizani mkaingie katika nuru yake ya ajabu."

Natumai ya kuwa,,umelipata fundisho zuri tena zaidi kupitia kwa somo hili la leo. Mungu na Akubarika sana,,,Amina!

Ombi.....

Mungu Mkuu na tena Uliye tukuka Juu ya vyote na yote,,tunakushukuru kwa ajili ya fundisho hili la leo.Kwa kweli tutalizingatia kupitia kwa usaidizi wa Roho wako Mtakatifu.

Ni kwa Yesu tumeomba.....Amen.....

Rafiki yangu,,hiki Kimekuwa ni kipindi chako cha kujifunza neno Lake Mwenyezi Mungu. Kipindi cha matumaini kutoka Twr.Leo mada yetu imekuwa ni swali ya kwamba;Je!,mimi ni mlinzi wa ndugu yangu?.

Tumeutoa kwenye Mwanzo 4:1-16.

Nitakuomba uwasiliane nami kupitia kwa anwani nitakayo kusomea mwishoni mwa kipindiki hiki cha leo. Anwani hiyo ni kwa ajili ya kusaidiana nawe.

Kabla yake,,u hapa wimbo mpende mwenzio,, ...

WIMBO.....

Na kwa kweli kabisa ni vyema kuwa mtu wa kuyazaa matunda mema na mwenye upendo kwa wenzako,,hao wakiwa ni wana-Huduma Revival church....Asante sana kwa wimbo huyo wa kutia Moyo.

ANDIKA BARUA AU UJUMBE WAKO UKIANZA NA NENO MATUMAINI TWR NA

KUTUMA KWA:

SLP 21514 CODE 00505

NAIROBI KENYA x2

Simu/Sms 0721970520 x2

Barua Pepe-barua@twr.co.ke

Kwenye Youtube ni @twr.co.ke

Mungu na akubarki sana Msikilizaji popote ulipo na,, hadi wakati mwingine, jina langu ni Vincent Amara.....Kwaheri